JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

*Barua zote ziandikwe na kutumwa kwa:*
**Simu:** +255 262 965 732(Direct line)
Nukushi: +255 262 965 732
**Barua Pepe:** ded@sikongedc.go.tz
**Tovuti:** www.sikongedc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge
4 MTAA WA BOMANI
S.L.P. 70,
**45382 SIKONGE - TABORA**

**Unapojibu tafadhali taja** **07/08/2025**

**Kumb. Na HWS/M.10/15/108/46**

## YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI ZA MKATABA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge anawatangazia Wananchi wote wenye sifa kutuma maombi ya nafasi ya kazi za Mkataba kwa nafasi mbalimbali kama zilivyoainishwa hapo chini:-

### 1.0 Fundi Sanifu II(Umeme) (Nafasi 01)

**1.1. Sifa za Mwombaji**

i. Awe na Cheti cha ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne na kuendelea
ii. Awe na Stashahada ya Ufundi wa Umeme kutoka chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

**1.2. Masharti ya Ajira**

i. Ajira hii ni ya mkataba wa Mwaka 1.

**1.3. Mshahara.**

Kiwango cha Mshahara ni kadri ya makubaliano yatakayofanyika na Mwajiri.

### 2.0 Afisa Tehama Msaidizi II (Nafasi1).

**2.1. Sifa za Mwombaji**

i. Awe na Cheti cha ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne na kuendelea.
ii. Awe na Stashahada ya masomo ya compyuta kati ya moja ya fani zifuatazo;Uhandisi wa kompyuta/Mitandao/Mawasiliano na Elekroniki au Matengenezo ya Mifumo ya TEHAMA kutoka kwenye Taasisi/Vyuo vinavyotambuliwa na serikali.

**2.2. Masharti ya Ajira**

i.Ajira hii ni ya mkataba wa Mwaka 1.

**2.3. Mshahara.**

Kiwango cha Mshahara ni kadri ya makubaliano yatakayofanyika na Mwajiri.

### 3.0 Mtayarishaji Vipindi Msaidizi II(Producer) (Nafasi1)

**3.1. Sifa Za Mwombaji**

i. Awe na cheti cha ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne na kuendelea.
ii. Awe na Stashahada ya Uandishi wa Habari kutoka chuo kinachotambulika na Serikali

CamScanner

### 3.2. Masharti ya Ajira
i.Ajira hii ni ya mkataba wa Mwaka 1.

### 3.3. Mshahara.
Kiwango cha Mshahara ni kadri ya makubaliano yatakayofanyika na Mwajiri.

## 4.0 Fundi Sanifu II (Sauti/Sound) (Nafasi1)

### 4.1. Sifa Za Mwombaji
i. Awe na cheti cha ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne na Kuendelea

ii. Awe na Stashahada ya Ufundi wa sauti (Sound) kutoka chuo chochote kinachotambulika Serikalini

### 4.2. Masharti ya Ajira
i.Ajira hii ni ya mkataba wa Mwaka 1.

### 4.3. Mshahara.
Kiwango cha Mshahara ni kadri ya makubaliano yatakayofanyika na Mwajiri.

## 5.0 Mfanya Usafi (Nafasi 28)

### 5.1. Sifa Za Mwombaji
i.Mwombaji awe na Elimu ya Darasa la Saba na kuendelea

### 5.2. Masharti Ya Ajira
i.Ajira hii ni ya mkataba wa Mwaka 1.

### 5.3. Mshahara.
Kiwango cha Mshahara ni kadri ya makubaliano yatakayofanyika na Mwajiri.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE**

i. Mwombaji awe ni Mtanzania
ii. Mwombaji awe na Miaka 18 hadi 45
iii. Maombi yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya Darasa la saba, kidato cha nne, kidato cha sita, Astashahada (Cheti) na Stashahada (Diploma), picha mbili za passport size iliyopigwa hivi karibuni, maelezo binafsi (CV) ya mwombaji na namba ya simu inayopatikana wakati wote.
iv. Mwombaji Aambatanishe kwenye maombi ya kazi nakala za barua za wadhamini wawili wenye kitumbalisho cha Taifa au namba ya (**NIDA**) na wanaofahamika katika jamii
v. Mwombaji awe na kitambulisho cha Taifa au namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA).
vi. Mwombaji juu ya Bahasha aonyeshe nafasi aliyoiomba
vii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **02/09/2025 saa 9:30** Alasiri
viii. Maombi yote yawasilishwe kwa anuani ifuatayo: -

**Mkurugenzi Mtendaji (W)**
**S.L.P 70**
**SIKONGE**

Selemani M.Pandawe
Mkurugenzi Mtendaji (W)
**SIKONGE**

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA - SIKONGE

**Nakala:** Kwenye mbao zote za matangazo ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

CamScanner